

JINA \_\_\_\_\_ DARASA \_\_\_\_\_

SAHIHI \_\_\_\_\_ TAREHE \_\_\_\_\_

102

KISWAHILI

KIDATO CHA PILI

MUDA:  $2\frac{1}{2}$

### **MAAGIZO**

Karatasi hii ina sehemu tano A,B,C,D na E. Hakikisha umejibu maswali yote katika kila sehemu.

SEHEMU		UPEO	ALAMA
A	UFAHAMU	20	
B	USHAIRI	20	
C	FASIHI SIMULIZI	20	
D	MATUMIZI YA LUGHA	30	
E	ISIMU JAMII	10	
	<b>JUMLA</b>	<b>100</b>	

Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa.

## **A.SOMA KIFUNGU KIFUATACHO KISHA UJIBU MASWALI YATAKAYOFUATA**

Uchafuzi wa mazingira umekithiri licha ya maonyo ya mara kwa mara na shirika la mpango wa mazingira katika umoja wa mataifa. Miti imekatwa bila ya kuacha ardhi wazi. Viwanda navyo vyachafua hewa kana kwamba vina udhia na jua. Uchafu kutoka viwandani unamezwa na mito, maziwa na mabahari, hivyo kuhatarisha maisha ya viumbe na mimeaya majini.

Matokeo ya maovu haya ni mabadiliko ya hali ya hewa kote uimwenguni. Kiwango cha joto kimezidi kiasi cha kukithiri si watu si wadudu si wanyama. Isitoshe ule ukanda wa ozone unafifia kasi kama wingu mchana wa jua. Vivyo hivyo, mpangilio wa misimu umevurugika; majirahayatabiriki tena. Mintarafu ya hayo, shughuli za kilimo zimekuwa za kubahatisha na mara nyingi hupigwa chenga na mavuno kuadimika.

Maeneo mengi ulimwenguni yamekumbwa na mafuriko mabaya inio. Nchi kama Idonesia, Msumbiji na maeneo ya Amerika ya kati na kusini yameathiriwa sana na mafuriko. Watu na wanyama wameangamia na mali si haba kuangamia. Nchi ya Kenya iliwhi kukumbwa na mvua ya Elnino. Matokeo yake yaliathiri uchumi na maendeleo kwa kiasi kikubwa.

Bali na mafuriko kuna ukame unaosababishwa na ongezeko la joto. Nchi kama Kenya, Zambia, Zimbabwe na Mali zimekumbwa na ukosufu wa chakula kwa miaka mingi. Wasomi wa siasa na jamii wanasesma kuwa mizozo ya kijamii na kimataifa huenda ikazidi ikiwa mahitaji haya ya kimsingi yataendelea kuadimika. Kwa mfano, nchi ya Misriinatishia kuzozana na yejote atakayevuruga maji ya mta Nile.

Je, si twaweza kubadilisha halihii? Mashirika ya Umoja wa Mataifa yameandaa misururu ya mikutano kujadili swali hili. Wahusika hutoa mapendekezo kama vile kuhimiza watu kutumia ujuzi wa kisayansi na teknolojia kuhifadhi mazingira. Yafaa tutumie rasilmali zetu kama maji na nishati bila ubadhifuru wowote. Aidha wenye viwanda wahimizwe hata kwa sheria kupunguza uharibifu wa mazingira. Watumie mbini za kutumia taka kama malighafi kuunda vifaa upya. Inasemekana kwamba mataifa yaliyostawi huchangia pakubwa kwa uharibifu wa mazingira kuititia viwanda. Hivyo, wayasaidie yale yanayoendelea kwaujuzi na teknolojia za kutuza mazingira, wasivitenge kwani jifya moja haliinjiki chungu.

Sote tujifunge kibwebwe na kwa jino na ukucha tuhifadhi mazingira yetu. Ushirika na jitihada zahitajika la sivyo tutajutia matendo yetu baadaye.

## **MASWALI**

1. Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 1)
2. Eleza namna mbalimbali za uharibifu wa mazingira. (alama 3)
3. Taja athari za uharibifu wa mazingira. (alamal 4)
4. Kulingana na kifungu hiki, vipi tunavyoweza kuhifadhi mazingira? ( alama 3)
5. Taja mbinu tano za lugha zilizotumika katika kifungu hiki na uzitolee mifano mwafaka. (alama 5)
6. Eleza maana ya msamati huu kama ulivytumika katika kifungu hiki. (alama 4)
  - i. Simile
  - ii. Malighafi
  - iii. Kukirihi
  - iv. tujifunge vibwebwe

## **2.USHAIRI**

### **SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI**

Kwa jina lake jalia,muumba nchi na mbingu,  
Aloumba insia, na wengi viumbe chungu,  
Rabi Mola metimia, kwake hakuna tewengu.

Haki ya kwanza sikia, ni ibada kwake Mungu,  
Moliwa kusujudia, alompa njema fungu,  
Mtumwa au huria, hakiye sitiwe pingu.

Kisha haki ya kuishi, hata chini ya mvungu,  
Apewe hakiye ghushi, mweusi hata mzungu,  
Kusiwe na kishawishi, kutengwa ja nyama nungu.

Haki nyingine apewe, ya hakiye toka tangu,  
Uhuru aachiliwe, hata apandapo dungu  
Maoniye ayatowe, si hoja ya dungudungu.

Na haki ya kumiliki, mja asiliwe bangu,  
Shamba lake la iliki, alolima kwa uchungu,  
Mtu asimdhihaki, kumpoka kwa manjungu.

Hakiye muhimu sana, ya jadi mithili nyungu,  
Ni mja kutangamana, na wenzi wacheze gungu,  
Kusiwe kubaguana, kupikana majungu.

Afungwapo gerezani, pwagu wa ndizi mkungu,  
Asitiwe matesoni, kuvunjwa mbavu na wengu,  
Mlo usiwe majani, kijisima na videngu.

## **B.MASWALI**

- 1. Andika kichwa cha shairi hili. (alama 1)**
  
  
- 2. Taja haki nne zilizotajwa katika shairi. ( alama 4)**

3. Liweke shairi hili katika bahari mbili na utoe sababu. (alama 2)
4. Taja mifano mitatu ya uhuru wa mshairi iliyotumika katika shairi hili na utoe mifano. (alama 3)
5. Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 3)
6. Taja mbinu tatu za lugha zilizotumika katika shairi hili na utoe mifano. (alama 3)
7. Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)

**C..FASIHI**

1. Andika tofauti tano kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. ( alama 5)
2. Jadili sifa tano za mtambaji bora. ( alama 5)

3. Fafanua vipera hivi vya fasihi simulizi: ( alama 5)
  - i. Mighani
  - ii. Maghani
  - iii. Vitendawili
  - iv. Hurafa
  - v. Nyiso
4. Eleza dhima za vipera vya nambari ya (3) ( alama 5)

#### D.MATUMIZI YA LUGHA

1. Taja irabu mbili za nyuma. (alama 2)
2. Eleza maana ya silabi zifuatazo na utoe mfano mmoja mmoja. ( alama 3)
  - a. silabi mwambatano
  - b. silabi fungo
3. (a) Eleza maana ya kiambishi. ( alama 1)  
(b) Taja aina za viambishi. ( alama 2)

- (c) Ainisha viambishi katika neno hili: ( alama 4)  
aliyempata
4. Eleza maana mbili za sentensi hii: ( alama 2)  
Wanafunzi waliwaimbia walimu.
5. Andika katika usemi halisi. ( alama 3)  
Mwalimu mkuu alitaka kujua kama walikuwa wamelipa karo yote ya muhula huo.
6. Eleza matumizi ya kisarufi ya neno –zuri katika sentensi hizi. ( alama 4)
- Uzuri wake ulimfanya kutolipiza kisasi.
  - Mazuri yaliuziwa waliokuwa na kiu.
  - Aliandika vizuri hadi akatuzwa.
  - Nilitaka tuhamie mahari pazuri zaidi.
7. Yakinisha sentensi hii: ( alama 2)  
Wasipojiandaa ipasayo wakati huu, hawatapita mtihani huu.
8. Andika katika hali ya ukubwa, wingi. ( alama 2)  
Mbuzi na ng'ombe waliuziwa wanawake hao.
9. Unda aina za nomino zilizo mabanoni kutoka kwa neno ulilopewa. ( alama 2)
- choka (dhahania)
  - mwandiko (kitenzi jina)
10. Andika aina tatu za vitenzi na utungie sentensi moja kila aina. ( alama 3)

## **E.ISIMU- JAMII**

**BOKONO:** (Wimbo) Ni ya leo, ni ya leo.

**ZENA:** Unauza nini?

**BOKONO:** Dada kama uavyoona, kuna mavazi poa ya baba, mama na watoi. Everyone. Wote wang'are.

**ZENA:** (Anachagua mini sketi)Hii ngapi?

**BOKONO:** Soo moja.Bei ya kuongea. Dada endelea kuangalia, kuona ni bure hata kupima ni sare.

**ZENA:** Nina hamsini pekee.

**BOKONO:** Ongeza pauni dada tafadhari.(Zena anaanza kuondoka) Kastoma tafadhari usiondoke. Kunja . Tutashikirishana.

## **MASWALI**

1. Tambua sajili hii na utoe sababu. ( alama 2)
  
2. Jadili sifa za sajili hii. (alama 8)